TOLEO NO.71

# Khilafah

SHA'ABAN 1447 HIJIRIA —FEBRUARI 2026 MILADIA ( Bei Tsh 4,000/= - Ksh 200/=) NDIO SULUHISHO

## WAISLAMU NA MATAYARISHO YA RAMADHANI



Kwa kuwa tumo ndani ya mwezi wa Shaaban hapana shaka wiki chache zijazo Waislamu tutakuwa na mgeni mtukufu, yaani mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Ramadhani ni mwezi wa Qur-ani, una usiku mtukufu, ndani yake hufunguliwa milango ya pepo, kufungwa milango ya moto, amali za Waislamu hulipwa maradufu na nyoyo za Waumini hulainika kwa kupanda juu ucha-Mungu wao, ukarimu na mapenzi baina yao.

Swala linakuja, jee Waislamu tuna maandalizi yeyote kwa ajili ya mwezi huu mtukufu? Allah Taala anataka katika mambo yetu tuwe na maandalizi Aliposema:

وَلَوْ أَرَادُوا الْخُرُوجَ لَأَعَدُّوا لَهُ عُدَّةً

"Na ingelikuwa kweli walitaka kutoka (kwenda vitani) bila ya shaka wangejiandalia maandalizi (makubwa)……" (Tawba: 46)

Bila shaka Waislamu hawako nyuma katika kujiandaa na Ramadhani katika mambo mbalimbali kama futari, kutafuta nguo za sikukuu, kukarabati misikiti, kuandaa maimamu wa tarawekhe nk.

Hata hivyo, Ramadhani inahitaji matayarisho nyongeza zaidi ya hayo yaliyozoeleka.

**Awali** kabisa, ni kumuomba Allah SWT Atufikishe kuidiriki Ramadhani, kwani wema waliotangulia (maswahaba) walikuwa ikimaliza tu Ramadhani wakimuomba Allah SWT Awakubalie funga na ibada zao. Na ukianza tu mfunguo saba walikuwa wakimuomba Allah Taala awafikishe waidiriki Ramadhani ijayo wakiwa na afya njema ili wanufaike na manufaa makubwa ambayo hayapatikani katika miezi iliyobakia.


**Pili,** Waislamu ni kujifunza masuala ya msingi kuhusu funga. Yaani wajue nguzo zake, mambo yanayobatilisha

**Inaendelea Uk. 3**

## Yaliyomo :


- **Ramadhani iko safi isichafuliwe**……………………………………… 2
- **Rai za Kifiqhi katika Kulipa Funga**………...…………………………4
- **Kubadilishwa Qibla ni msimamo katika hukmu za kisharia** …….5


## NYARAKA ZA KASHFA YA EPSTEIN



Kiasi wiki moja nyuma (30/1/2026) Wizara ya Haki ya Marekani imeweka hadharani mafaili ya aliyekuwa bilionea maarufu Jeffrey Epstein. Mafaili yenye kurasa zaidi ya milioni tatu na nusu, video 2000 na mapicha laki moja na elfu themanini. Yote hayo yakionyesha unyama, ushenzi na ukatili wa kupindukia uliokuwa ukitendeka kwenye Kasri la Bwana Epstein katika kisiwa chake huko virgin Island, Marekani.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari mafaili hayo yamedhibitiwa kwa kuondoshwa baadhi ya mapicha na video kadhaa zinazowahusu wanasiasa maarufu akiwemo rais wa sasa wa Marekani Donald Trump.

Bwana Epstein alikuwa tajiri aliyejihusisha na biashara ya wanadamu ya vitoto vidogo vya kike umri kati ya miaka

**Inaendelea Uk. 5**

## RAMADHANI IKO SAFI ISICHAFULIWE

Moja katika madhara makubwa ya kuangushwa dola ya Kiislamu ya Khilafah ndani ya mwezi wa Rajab 1342 Hijria/ Machi 1924 ni ibada za Kiislamu kukosa msi-usimamizi, hali iliyopelekea ku-geuzwa kuwa mambo ya mizaha na kuchezewachezewa kama kitu kisicho na maana yoyote.

Kuchezewa huku ibada zetu kunahusisha kupotoshwa mafhumu yake ya asili. Kwa mfano, ibada ya jihadi ime-geuzwa kwa kila kitu kuwa ni'ji-hadi' badala ya ufahamu wake wa asili ambao huhusisha vita vya moto na yenye uhusiano nayo moja kwa moja.

Ibada nyengine kama Hijja imetengezwa mazingira ya uzito usio na mfano katika masharti, gharama nk.

Bali pia ibada nyengine kama Swaumu ya Ramadhani hudogoshwa na kufanywa kama upuuzi badala ya kubakia katika nguvu na hadhi ya ibada hizo kama zilivyoletwa katika uasili wake.

Wakati tukiwa katika mwezi wa Shaaban tukijiandaa kuingia katika mwezi wa kheri, baraka na utukufu mkubwa tuna-shuhudia pia maandalizi ya kui-haribu na kuichujua ibada hiyo.

Ibada ya swaumu ya Ramadhani kwa bahati mbaya sana hutumi-ka vibaya kuwa jukwaa la kupig-ia debe fikra hatari ya 'dini mseto' . Wakati mwengine kui-wasilisha ibada hiyo kana kwam-ba inawahusu hata wasiokuwa Waislamu.

Aidha, ibada ya Swaumu hugeu




zwa kuwa ni chombo cha kui-marisha fikra ya usekula. Fikra inayohubiri dhana ya kumfunga Mwenyezi Mungu katika mae-neo maalum. Yaani huoneshwa kana kwamba Ramadhani ndio mwezi wa Ibada, na isiyokuwa Ramadhani kana kwamba sio lazima kuwa na uchamungu.

Mtazamo huo huanza kudhihiri-ka mapema ndani ya mwezi ka-ma huu wa Shaaban kwa kudan-dia fikra hatari na batil ya 'vunja jungu' ambayo hulenga kufanya haraka kutenda matendo maovu yaliyoharamishwa na Uislamu katika dakika za mwisho hu-susan siku chache kabla ya kuin-gia Ramadhani, matendo am-bayo ni vigumu kuweza kuyatenda kwa usahali ndani ya Ramadhani, (japo ukweli maten-do hayo huwa yamekatazwa wa-kati wote).

Matokeo ya fikra ovu ya 'vunja jungu' ni watu wakiwemo baadhi ya Waislamu kimakosa kujitosa katika maovu na maasi mbalimbali kinyume na Uislamu siku chache kabla ya Ramadhani. Pia Ramadhani hutumika viba-ya na wanasiasa wa kisekula kwa kwa kuitumia kwa matangazo yenye nia ya kujinufaisha kisiasa au kiuchumi kupitia mgongo wa ibada hiyo. Kwa mfano, baadhi ya wanasiasa huandaa futari kwa wao wenyewe kushiriki au

kutuma wawakilishi wao, kisha kutajwa majina ya vyama vyao au kufikishwa maagizo yao kwa jina la salamu za Ramadhani kutoka kwao.

Mwaka huu tunashuhudia wanasiasa hao wakija na ajenda ya shamra shamra za kuwa na mashindano maalumu ya mpira wa miguu kwa jina la kombe maalumu la Ramadhani.

Lengo la mashindano hayo ni kuwashughulisha Waislamu, kuondoa ladha ya Ramadhani, bali hata kuwafanya baadhi was-ifunge kamwe !

Tunasema bayana na kwa kin-ywa kipana kwamba ibada ya swaumu ni ibada adhimu kwa ajili ya Waislamu tu, kwa ajili ya kuvuna uchamungu na kujita-kasa mbele ya Mola wao, ibada hiyo iko mbali na mizaha, michezo na upuuzi na haina uhusiano wowote na siasa za kisekula na wafuasi wake.

Basi kama ilivyokuwa ibada hiyo kuwa mbali na hayo, basi tunamwambia kila mwenye malengo kwa Ramadhani kin-yume na Uislamu atuwachie iba-da yetu.

**Mhariri**

**Sha'aban 1447 Hijria**

**Februari 2026 M**

***jukwalakhilafah@gmail.com***

*************

## Matayarisho ya Ramadhani... *kutoka uk .1*

kusihi kwake nk. ili mfungaji awe na uhakika kielimu wa anachokitenda. Na kama Muislamu hujui basi ni lazima ajiegemeze kwa mwanazuoni Mujtahid ili iwe hujjah kwake kuwa katekeleza ibada hiyo kwa elimu. Allah SWT kutukataza kutekeleza jambo tusilo na elimu nalo, maana yake ni kuwa jambo hilo tulitafutie maarifa yake. Tumeshuhudia Waislamu hujifunza kwa haraka kuhusu Hijja miezi michache kabla ya safari. Basi na kwa Ramadhani hilo linawezekana.

**Tatu,** Waislamu katika kipindi hiki tunapaswa kujiandaa kwa kuhakikisha hawazidhulumu nafsi zao kwa kufanya maovu na badala yake wanaziokoa nafsi zao kwa kuhakikisha wanajiweka safi kuingia katika mwezi mtukufu wakiwa safi ili kumridhisha Allah Taala pekee kwa kuheshimu matukufu yake. Allah SW anasema:

ذَٰلِكَ وَمَنْ يُعَظِّمْ شَعَائِرَ اللَّهِ فَإِنَّهَا مِنْ تَقْوَى الْقُلُوبِ

"Ndio hivyo! Na anayetukuza matukufu ya Mwenyezi Mungu, basi hayo ni katika uchamungu wa nyoyo" (Hajj: 32)

Nne, Waislamu hatuna budi kujiandaa kifikra na kisaikologia kabla ya kuingia Ramadhani, kwa kuweka azma ya kweli, kuifunga Ramadhani yote kwa ikhlasi na unyenyekevu na kujiweka mbali na shubha zote. Pia tujiepushe kuipokea Ramadhani kama jela au kero fulani. Aidha, tujiepiushe kufunga tu ilimuradi watu watuone, au kuogopa kusemwa vibaya ndani ya jamii. Mtume SAAW anatufundisha kuwa vitendo vitalipwa kwa kuzingatia nia ya mtendaji.

Tano, matayarisho pia yanahusisha kwa Waislamu kuanza kujizoesha kufanya ibada mbalimbali ili isije kuwawia ugumu kwao kuzitenda ibada hizo itakapoanza Ramadhani. Ni vyema kuanza kufanya baadhi ya ibada kama qiyamullayli, kusoma Qur-ni Tukufu kwa kuuzoesha ulimi, kufanya dhikri mbali mbali, kutoa sadaka nk.

Bibi Aisha ra. anasimulia kuwa Mtume SAAW alikuwa akifunga zaidi mwezi wa Sha'abani mpaka unadhania hafungui ataunganisha na Ramadhani…". Sasa kwetu ni vizuri kuiga mwendo huo mzuri, kama ni matayarisho kwa ibada hii.

Kwa kumalizia, maandalizi ya Ramadhani yana wigo mpana, hivyo, kila jambo jema ambalo litafanya ibada yetu hiyo iwe na ufanisi hatuna budi kuliweka tayari tayari ili kufanikisha ibada hiyo adhimu inayokuja wiki chache zijazo inshaAllah

Imeandikwa na Ali Amour

Mjumbe wa Afisi ya Habari- Hizb ut Tahrir Tanzania.

****************




## Kashfa ya epstein … kutoka uk 1

kumi na kitu hadi chini ya miaka 18 na kuwapeleka katika kisiwa chake na kuwatumikisha kingono, kuwalawiti, kuwabaka, kuwapa mimba, na hata kuwaua!

Mafaili na kurasa hizi za bwana Epstein zimewahusisha wakishiriki katika vitendo hivi vya kinyama wanasiasa kadhaa ulimwenguni wakiwemo marais wa Marekani Bill Clinton, Joe Biden, Obama pia bibi Hillary Clinton na watu wengine maarufu na matajiri duniani kama Bill Gate, Elon Musk, Profesa Stephen Hawkins, mwana Mfalme wa Uingereza Andrew na baadhi ya watu mashuhuri pia katika bara Arabu.

Mapicha na video nyengine katika mafaili haya yakiwaonyesha hata wanasiasa hao wakubwa wakifanyiana wao kwa wao vitendo vya kashfa na ushenzi!

Yote hayo yakitendeka katika tafrija mbalimbali katika Kasri la Bwana Epstein katika kisiwa chake huko Marekani na akirekodi kila kitendo na tukio humo kupitia kamera alizozifunga kila eneo kwenye kisiwa hicho. Na pia akiweka kumbukumbu za maandishi.

Wasichana na watoto wadogo wakike walidhalilishwa kinyama na mamia ya wahanga waliosalimika kuuawa wamekuwa wakijitokeza huko Capitol Hill na kwengineko Marekani kupaza sauti zao wakidai hatua zichukuliwe dhidi ya waliowadhalilisha kinyama na kila kitu kiwekwe hadharani.

Epstein alishikiliwa gerezani na

**Inaendelea uk 7**

# RAI ZA KIFIQHI KATIKA KULIPA FUNGA

**Swali:**

Asalaam Alaykum Warahmatullah Wabarakatuh,

Nilikuwa katika jahiliyyah na kwa makusudi nikaacha funga ya Ramadhani bila ya udhuru, kisha, Alhamdulillah Allah Akanirehemu nikatubu, vipi nilipe funga niliyoiacha? Je ni juu yangu kulipa fidia kila mwaka au inatosha kulipa tu?


**Jawabu:**

Waalaykum Salam Warahmatullah Wabarakatuh,

Ndugu yangu mesema ulikuwa hufungi kwa muda mrefu tena kwa makusudi bila ya udhuru wa kisheria. Kisha baada ya miaka hiyo Allah akakuongoza kwenye njia iliyonyooka ukawa unafunga huli mchana… Na kwasababu ya uchamungu unataka kulipa miezi ya Ramadhani zilizopita ambazo hukufunga … Namshukuru Allah kuwa amekuongoza kwenye utiifu mzuri kiasi ambacho hukutosheka kufunga tu baada ya Allah kukuongoa, bali una pupa la kulipa miezi ya Ramadhani ambayo hukuifunga. Allah akubariki, aifanye njema toba yako na akuenezee neema zake na rehema zake.

Sisi hatutabanni katika ibadati bali tunaliacha jambo kwa Muislamu mwenyewe afuate madhehebu yoyote katika funga au swala…nk. Mimi hapa nitakutajia baadhi ya rai za kifiqhi katika kulipa funga, na utachowafiki unaweza ukafuata:

1-Imeelezwa katika kitabu kitwacho *"Nihaayatul-Mutwalib fi diraayatil-Madhaahib"* cha



Aljiweyni, (Imamul-Haramain) (aliyefariki 478H), katika fiqhi ya Shafi:

(Mwenye kupitwa na funga ya Ramadhani kwa masiku kadhaa, na akapata uwezo wa kuzilipa, basi haifai yeye kuchelewesha kuzilipa mpaka (ukaingia) katika mwaka ujao, hili tunalolitaja si Sunna bali ni la lazima, ila awe anaweza na nyudhuru ziwe zimeondoka. Na kama itakuwa kuchelewesha kulipa mpaka mwaka ujao bila ya udhuru basi itakuwa kulipa pamoja na kibaba cha chakula kila siku, na kama atachelewesha kulipa kwa miaka miwili au miaka kadhaa, ongezeko la fidia litakua kwa njia mbili: Moja ni kwamba haiongozeki, na wala si wajibu kuchelewesha kwa miaka kadhaa isipokuwa kwa kilichowajibu (ikabidi kuchelewesha) hata kwa mwaka mmoja… na lililosahihi hasa katika hali hii ni kuongozeka kwa fidia na kuifanya upya, kwa hiyo ni wajibu kwa kuchelewesha kwa kila mwaka (kutolewa) kibaba. Basi akichelewesha miaka miwili, ni wajibu vibaba viwili kwa kila siku anayolipa, hivi ndivyo inavyozidi na kuendelea hivi ndivyo inavyozidi na kuendelea. (Huu ndio msimamo katika fidia…). Hii ina maana kwamba kulipa funga ya

Ramadhani kwa asiyefunga ailipe kabla ya Ramadhani ijayo na akichelewesha mpaka baada ya kuingia Ramadhan (nyengine) basi juu yake kulipa na kutoa fidia… Na ana rai nyengine, nayo ni kwamba kwa mfano, akichelewesha kulipa kwa miaka miwili atawajibika kulipa pamoja na fidia mbili. Hali iko hivyo.

2-Ama katika madhehebu ya Abuu Hanifa ni kuwa, kwa namna yoyote atayochelewesha kulipa hawajibiki (kutoa fidia) isipokuwa ni kulipa tu, ikiwa itafika Ramadhani nyengine… atalipa ile iliyompita na wala hawajibiki fidia kwa kuchelewesha:

3-Imeelezwa katika kitabu cha *Almabsuut* cha mwandishi Al-Sarkhasy aliyefariki mwaka 483H (Fiqhi ya Kihanafi)

Amesema: (Mtu ambae ana wajibu wa kulipa masiku katika mwezi wa Ramadhani na akawa hakulipa mpaka ikaingia Ramadhani ijayo… ni juu yake kulipa Ramadhani iliyopita na wala hatolipa fidia kwa mujibu wa rai yetu. Na kwa mujibu wa Shafi Allah amrehemu, analazimika kulipa pamoja na kulisha masikini kwa kila siku… Sisi tuna (tumeshika) dhahiri ya kauli ya *Taala*: ***"Basi atimize idadi yake katika masiku mengine"*** (Albaqara:184). Hamna humo hapajatajwa muda maalumu wa kulipa). Kuweka muda maalumu ni baina ya Ramadhani mbili. (ziada, na hii ni ibada iliyoekewa wakati maalumu lakini kuilipa haijawekewa muda maalumu..)

**Inaendelea uk ..6**

kufia humo (ikidaiwa kuwa kajiua) mwaka 2019 akisubiri kesi yake ya biashara ya wanadamu ya kuwatumikisha kingono.

Ila wachambuzi wanasema aliuliwa makusudi kwa mipango ya wahusika wakubwa wa Marekani ili kuficha kashfa nyingi za wanasiasa na matajiri wakubwa ambazo zingefichuka.

KINACHOJIRI WAZI KATIKA KASHFA HII YA EPSTEIN:

Allah anasema:

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ لَا تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ قَالُوا إِنَّمَا نَحْنُ مُصْلِحُونَ. أَلَا إِنَّهُمْ هُمُ الْمُفْسِدُونَ وَلَٰكِن لَّا يَشْعُرُونَ

***"Wanapoambiwa msifanye uharibifu duniani wao husema sisi tunatengeneza. Tambueni hao ndio waharibifu lakini hawaelewi"***

Kadhia hii imedhihirisha mambo kadhaa muhimu kwetu Ummah wa Kiislamu na ulimwengu kijumla:

**1. KUFELI KWA MFUMO MZIMA WA UBEPARI:**

Kama kawaida yao wanasiasa wamagharibi, kinachojitokeza masiku haya ni kupumbaza akili za watu kuwa tatizo ni mtu au watu fulani waliohusika na unyama huu. Lakini ukweli ni kwamba tatizo ni mfumo mzima wa Kibepari ndio umefeli kutoka msingi wake na namna unavyoyatazama maisha na kipimo cha matendo ya mwanadamu maishani. Maisha kwao ni mwanadamu atakavyojipangia na ndio wakachagua ubepari na msingi wake wa kisekula, na ikawa furaha kwao ni mwanadamu kuchukuwa sehemu kubwa ya starehe apendayo ili ajiridhishe. Kwa hiyo ikiwa kulawiti, ubaradhuli, ubakaji, ulevi, umalaya, uzinifu, kutembea utupu nk vitampa starehe mwanadamu hiyo ni furaha na lazima aitende na hakuna wakumzuia na sheria yao itamlinda.

Kipimo cha vitendo maishani, kwao imekuwa ni maslahi tu, si kitu kingine. Kwahiyo unyama wote uliokuwa unatendeka katika visiwa vya Epstein ni sura halisi ya mfumo wa ubepari na wala si bahati mbaya eti waovu tu akina Epstein na akina Trump na akina Clinton na akina Bill Gate, Bill Cosby, Michel Jackson, Jay Z, P Diddy na wengineo. Hawa wote na matendo yao ambayo yamezagaa si tu Marekani bali Ulaya na kwengineko ni zao la mfumo huu wa ubepari uliofeli. Maovu haya yote katika mfumo huu ni ya kawaida kwa yanawapatia furaha na mapesa. Na ndio ikawa sanaa ya ngono na zinaa na ulevi ni kazi halali kwao. Na ndio rais Clinton mwaka 1997 akapata kashfa kubwa ya uzinzi na mfanya kazi wake ikulu bibi Monica Lewinsky. Na ndio katika uchaguzi wa Marekani wa 2019, Meya aitwae Pete ambae ni baradhuli alishiriki kinyang'anyiro cha urais!

**2. KATIKA DEMOKRASIA WANASIASA NA MABEPARI WAKO JUU YA SHERIA**

Si kweli msemo wa wamagharibi kuwa hakuna alie juu ya sharia. Ukweli ulio wazi ni kwamba binadamu ndie alietunga sheria na wakati wote anahakikisha inalinda maslahi yake. Kesi hii ni ya muda mrefu, kwanini wakaondoa baadhi ya taarifa kwenye mafaili haya?! Yote ni kuwalinda mabepari wakubwa na wasiasa wakubwa akiwemo rais wa sasa wa Marekani bwana Donald Trump. Rais huyuhuyu Trump mwezi wa Januari mwaka jana hakimu Juan Merchan jijini New York alimfutia mashtaka yake yote 34 ya jinai aliyokuwa nayo kwa hukumu aliyoiita jaji huyu kuwa "unconditional discharge"! Makosa dhidi ya Trump yalithibiti lakini alilishia na kubwa zaidi ilikuwa ni kuepusha fedheha ya kutiwa jela au kutozeshwa faini rais mteule wa taifa kubwa la Marekani. Hata majuzi tu kitendo cha aibu cha kuvunja sheria zao za kimataifa kilifanya na taifa hili la Marekani kuvuka mipaka ya nchi huru yenye mamlaka na kuingia na kumkamata rais wake, Maduro. Ucheleweshaji wa kuwekwa wazi mafaili haya hadharani na kitendo cha kuondoa baadhi ya taarifa kutoka mafaili haya zisitokee hadharani, yote haya ni kuwalinda walio juu ya sheria mabepari wakubwa kina Elon Musk, Bill Gate, Trump na wengineo.

3. DEMOKRASIA SIO KWELI KUWA INALINDA HAKI ZA WATOTO

Yaliyofichulia katika nyaraka hizi za Epstein dhidi ya watoto watoto wadogo yalikuwa yakitendeka huko tangu miaka ya 1995 alipoanzisha unyama huu bwana Epstein, lakini hakuna

**Inaendelea uk ...7**

**Kubadilishwa Qibla…** *kutoka uk .5*

tutaulizwa na Muumba juu ya utekelezaji huo.

Suala la uteremshwaji wa sheria, kama vile muda, munasaba, namna Allah Taala alivyoziteremsha nk. kamwe halihusiani na wanadamu wala halipaswi kuwa hoja au dalili kwa namna yoyote kulifungamanisha na namna ya utekezaji. Hii ina maana kuwa, mara hukmu ikishushwa na Allah Taala, kwetu huwa ni wajibu kuitekeleza kimsingi/radical bila ya kutoa kisingizio kwamba twaweza kuitekeleza kidogo kidogo. Suala la uteremshaji ni kando na utekelezaji, na hilo ni elimu ya Mteremshaji na sio zaidi.

Pamoja na mifano mingi ya jambo hilo namna masahaba walivyozitekeleza hukmu kimsingi mara zilivyoteremshwa. Tukio hili la qibla ni mfano hai na wa wazi zaidi.

Mtume SAAW alibadilisha qibla akiwa ndani ya swala, hata hakusubiri kumaliza swala hiyo, baada ya Allah Taala kumtaka abadilishe. Ndio maana hadi leo kuna Msikiti unaoitwa Masjid Qiblatain huko Madina, kwa kuwa Mtume SAAW aliwaswalisha Waislamu swala moja kwa kutumia vibla viwili.

Nne, katika tukio hili kuna mazingatio ya kuzifikisha hukmu za kisharia kwa wengine bila ya kutafuna maneno. Tunaona wale waliooswalishwa na Mtume SAAW kilipobadiliswa Qibla ndani yake, waliporudi tu katika maeneo yao kando kidogo na kuwakuta baadhi ya Waislamu bado wanaswali, haraka nao waliwaeleza Waislamu hao wakiwa bado ndani ya swala kuwataka wabadilishe qibla mara moja. Hayo ni kwa sababu masa haba walielewa uwajibu wa kuifikisha hukmu kwa wengine ili itekelezwe kivitendo, kwa kuwa haikuletwa kuwa ni nadharia. Bali pia walijua utekelezaji wa hukmu inapokuja ni mara moja bila ya kusita sita.

Imesimuliwa katika Hadithi ya Barr Ra. katika Sahih Bukhar aliposema:

وَصَلَّى مَعَهُ رَجُلٌ الْعَصْرَ ثُمَّ خَرَجَ فَمَرَّ عَلَى قَوْمٍ مِنْ الْأَنصارِ فَقَالَ هُوَ يَشْهَدُ أَنَّهُ صَلَّى مَعَ النَّبِيِّ فَانْحَرَفُوا وَهُمْ رُكُوعٌ فِي صَلَاةِ الْعَصْرِ»

***" (Siku kilipobadilishwa kibla)…… Na aliswali asri (Mtume SAAW) pamoja na watu, kisha akatoka mtu na akapitia watu wa Ansar na akasema, kwamba yeye anashuhudia kuwa aliswali pamoja na Mtume (SAAW) na kuwa ameelekea alkaaba. Basi waliokuwa wakiswali wakageuka wakiwa katika rukuu katika swala ya asri''.***

Kwa kumalizia, katika hali ya leo ambapo tayari hukmu zote zimeshateremshwa ni wajibu Waislamu kuzitekeleza zote. Amma zile zinazohusiana na nguvu ya kidola, ni wajibu dola ya Kiislamu ya Khilafah kuzitekeleza mara moja inaposimamishwa dola hiyo InshaAllah. Hili ni sharti la msingi kwa dola ya Khilafah, yaani kutekeleza hukmu zote bila ya kuacha hata moja.

Hii ni dalili kuwa madola kama Saudia, Iran, Sudan na mfano wake si madola ya Kiislamu. Kwa kuwa si tu yanaendelea kuwadhuru Waislamu wazi wazi, bali pia hayatekelezi hukmu zote za Kiislamu ipasavyo. Hivyo, ni wajibu kwa Umma wa Kiislamu kufanya kazi kumtawalisha mtawala mmoja atakayetawala kwa sharia zote kwa ujumla wake kama unavyowajibisha Uislamu. Utawala unaopaswa kuanzia katika ulimwengu wa Kiislamu na kuenea mashariki na magharibi.

**Kulipa Swaumu….uk..4**

**4-**Na imeelezwa katika kitabu cha *Badaaiu Al-swanaaiu fii tartiibi Al-sharaai'i* cha Alau Diin Alkaasaany Alhanafi (Aliyefariki mwaka 587H):

(…madhehebu ya wenzetu – wanavyuoni wetu – ni kwamba wajibu wa kulipa hauna wakati maalumu, kutokana na kile tulichoeleza kuwa jambo hili la kulipa ni mutlaq halina wakati maalumu. Kwahiyo, liende hivyohivyo kwa itlaaq yake. Na kwahivyo wamesema wenzetu kuwa Muislamu atakapochelewesha kulipa Ramadhani mpaka ikaingia Ramadhani nyengine hatotoa fidia…). Hii ina maana kwa mujibu wa madhehebu ya Abu Hanifa kilichowajibu ni kulipa tu bila fidia, yaani atalipa miezi ambayo hakufunga tu.

Na kama nilivyosema awali, sisi hatutabanni katika ibadat, nilichokutajia ni baadhi ya rai za madhehebu. Linalokua wazi katika kifua chako basi lifanye… Allah akuwafikishe kwa alipendalo na kuliridhia.

Nataraji haya kuwa yametosheleza. Na Allah ni Mjuzi zaidi na Mwenye hekima zaidi.

**Ndugu yenu Ata Ibn Khalil Abu Rashtah**

**08, Ramadhani 1440H**

**13, Mei 2019M**

aliyefumbua mdomo kuyadhukuru na ili kuwalinda watoto hawa wadogo waliokuwa wakinunuliwa na kuhadaiwa wakafanye kazi nzuri watapata pesa kitita. Watoto wasiojua mbele wala nyuma wala hawana uwezo wa kufanya maamuzi, bali ilikuwa wengi wao umasikini wao tu, wengine waliacha mashule na vyuo wakidhani watapata kweli vitita vya kujikimu na wazazi wao kumbe waliishia kunyanyaswa kijinsia, kulawitiwa, kutiwa mimba na hata kuuliwa na kutoweka moja kwa moja. Bali wasimamizi wa haki za watoto ndio waliokuwa washiriki katika tafrija za furaha watoto hawa wahanga wakitendewa unyama huu mbele yao huku wakicheka, bali nao pia kutenda kama nyaraka zinavyosema kuwa bwana Trump alimpa mimba mtoto wa miaka 13.

Demokrasia hailindi haki za watoto bali inakanyaga haki zao na kuwadhalilisha na kuwapoteza. Leo hii duniani kwa mujibu wa takwimu za UN watoto milioni 8 kila mwaka wanatoweka. Marekani pekee ni laki nane, Uingereza laki mbili elfu arobaini. Ziko wapi haki za watoto! Ni urongo mtupu.

**4. DEMOKRASIA HAILINDI HAKI ZA WANAWAKE BALI INAWATWEZA**

Yote yaliyojiri kwenye visiwa vya bwana Epstein ili yanoge ni kushirikisha wanawake. Walifanywa bidhaa za ngono. Hata bibi Hillary Clinton kaonekana kwenye mapicha akishiriki maovu haya, na wanawake wengi wangine maarufu kama aliyekuwa mke wa Bill Gate bibi Mellinda, bibi Sarah Ferguson aliyekuwa mke wa mwanamfalme Andrew, bibi Maxwell aliyekuwa mshirika mkubwa wa Epstein katika biashara hii chafu, Mette-Marit mwana malkia wa Norway, Mira Nair mwendesha filamu mkubwa, bi Kathryn Ruemmler aliyekuwa mshauri wa ikulu ya white house wakati wa Obama, mwanamalkia wa Sweden bibi Sofia, mke wa Trump – Mellania na wengio, wote wamehusishwa katika kashfa hii na kutajwa katika nyaraka zilizoanikwa hadharani.

Wanawake katika nidhamu ya demokrasia ni bidhaa na viumbe wasio thamani. Huanikwa hadharani utupu na kudhalilishwa. Ndio kivutio kikubwa na kichocheo kikubwa cha uovu wa zinaa duniani.

Swali, je hawa wahanga wanaojitokeza waliosalimika kuuawa katika kadhia hii Epstein kuna atakae wasikiliza na haki zao zitazingatiwa. Au patasemwa tu kuwa waliyotendewa ni maovu lakini hayawezi kuwa jinai na kesi kuendeshwa? Ni yaleyale ya wahanga wa Trump na jinai kupuuzwa na hatimae akachaguliwa kuwa rais.

5. UBEPARI ULIOZAA DEMOKRASIA NI UOZO NA UVUNDO

Kutoka msingi wake wa usekula kuwa haufai kwa kuwa haukujengwa juu ya akili bali ni suluhisho la kati na kati (compromise solution/watu wa dini wasiokose kitu na watu wa dunia wasikose pia lakini mirengo hii isiingiliane), ubepari na demokrasia vimekuwa wazi leo ulimwenguni havimfalii binadamu katika ustawi wake maishani na kulinda utu wake. Na havina chochote cha kuwapa wanadamu isipokuwa uzinifu, ubakaji, ulawiti, ulevi, mporomoko wa maadili, ujambazi, umalaya, dhuluma, ukoloni, vita vya wenyewe kwa wenyewe, mauaji na ukatili, udhalilishaji wa kijinsia, kamari, madawa ya kulevya, kadri tutakavyotaja, yote yatakuwa matunda tarajiwa ya mti na mzizi muovu wa Ubepari.

Allah amesema katika 14: 26

***"Na mfano wa neno ovu ni kama mti muovu upo juu ya ardhi hauna uimara"***

Ni Uilsamu pekee sasa ndio mbadala wa yote hayo. Mfumo uliojengwa juu ya msingi wake madhubuti wa Imani iliyojengwa juu ya akili razini na yenye kuwafikiana na maumbile yake mwanadamu. Mfumo ambao mtazamo wake maishani ni kumtumikia Allah Muumba na furaha ni lenye kumridhisha Yeye Muumba. Na kipimo cha matendo maishani sio maslahi bali ni analolitaka Muumba hutendwa na asililotaka Muumba huachwa kutendwa, yaani kipimo cha halali na haramu. Huu ndio mfumo utakao hifadhi utu na heshima ya mwanadamu awe mtoto au mtu mzima, awe mwanamke au mwanaume. Na ni mfumo utakao leta ustawi wa mwanadamu.

*****************

**SEMINA MAALUM YA RAJAB 1447 H**

**Taarifa kwa Vyombo vya Habari**

Jumatatu, 30Rajab 1447 H -19 Januari 2026 M

Na: 05/1447

# Hizb ut Tahrir / Tanzania Yafanya Semina kwa Mnasaba wa Kumbukumbu ya Miaka 105 ya Kuvunjwa kwa Khilafah

Katika kumbukumbu ya miaka 105 ya kuvunjwa kwa Dola ya Khilafah iliyotokea mnamo Rajab 1342 H / Machi 1924 M, jana, Jumapili, 29 Rajab 1447 H / 18 Januari 2026 m, Hizb ut Tahrir / Tanzania ilifanya semina fupi katika Masjid Taqwa, Ilala Bungoni, katika jiji la Dar es Salaam.

Semina hiyo iliyoanza saa 3 asubuhi hadi saa 6. mchana iliwahusisha washiriki 80 hasa Maimamu, Maustadh, Masheikh na watu wengine mashuhuri kutoka maeneo tofauti ya jiji la Dar es Salaam na viunga vyake.

Semina hiyo ilifunguliwa na Sheikh Mussa Kileo, Mwenyekiti wa Kamati Kuu ya Mawasiliano ya Hizb ut Tahrir Tanzania, ambapo mada tatu ziliwasilishwa: Khilafah ni nini? Kuvunjwa




kwa Khilafah, na Njia ya Kusimamisha tena Khilafah.Washiriki walipata fursa ya kuuliza maswali, kutoa maoni na kushiriki katika majadiliano kuhusu mada hizo, na walipewa nakala za kila mada pamoja na nakala ya hotuba ya hivi karibuni ya Amiri wa Hizb ut Tahrir, mwanachuoni mkubwa na sheikh Ata Bin Khalil Abu al-Rashtah, kwa mnasaba wa kumbukumbu hii mahususi.

Hatimaye, semina hiyo ilihitimishwa na Masoud Msellem, Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir Tanzania ambaye aliwasisitiza washiriki na Ummah wa Kiislamu kujiunga na Hizb ut Tahrir ili waweze kushughulika pamoja nayo katika kadhia nyeti ya faradhi ya kusimamisha tena Dola ya Khilafah ambayo inapaswa kuanza katika ulimwengu wa Kiislamu, ngao ya Waislamu na rehema kwa wanadamu wote.

Tunaomba kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu aruzuku washiriki wote thawabu nyingi, na kuifanya semina hii kuwa nyongeza ya mwamko zaidi na ushindi kwa Ummah wetu mtukufu. Amin.

**Masoud Msellem**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir**

